# MPANGO WA KUBORESHA MADUKA YA DAWA BARIDI NCHINI

(Accredited Drugs Dispensing Outlets – ADDO)

# 1. MADUKA YA DAWA BARIDI (DLDB)

## 1.1 HISTORIA

- Kuanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Sumu Na.9 ya mwaka 1978 na pia kanuni za 1990. Aidha, Mwongozo wa Uendeshaji wa DLDB, Mei 1998.

- Sheria ilitambua kuwepo kwa Dawa Moto/Dawa za daraja la kwanza (Part I Poisons or PoM) na Dawa Baridi/ Dawa za daraja la pili (Part II Poisons or OTC)

## 1.2: Lengo la kuanzishwa DLDB

Sababu: Kutokidhi kwa sekta ya dawa ya umma kutosheleza upatikanaji wa dawa za msingi nchini ambapo kulisababisha kukosekana hata kwa dawa za msingi (basic drugs) - vijijini

- ✓ Kuruhusiwa kuanzishwa kwa DLDB kwa maslahi ya Taifa
  - - Kuna na vibali/leseni
  - - Kusimamiwa kwa mujibu wa sheria na wataalam
  - - Kuuza dawa baridi pekee
  - - Mahsusi kwa ajili ya maeneo ya vijijini

## 1.3: Matatizo ya DLDB

Baadhi ya matatizo ya DLDB ni:-

- Kuuza dawa zilizoisha muda wake
- Kuwepo kwa wauzaji wa dawa ambao hawana utaalam/ujuzi wowote
- Kufunguliwa kwa DLDB sehemu za mijini tofauti na lengo la awali.
- Kuuza dawa zilizoibiwa kutoka miradi ya serikali mf. MSD, TB & Leprosy, EDP, MCH n.k
- Kuuza dawa zisizosajiliwa na zisizoruhusiwa kinyume cha sheria
- Kuendeshwa kwa DLDB bila kibali au leseni

- Kununua dawa kutoka katika vyanzo visivyofahamika na hivyo kutokuwepo na uhakika wa ubora wa dawa
- Kugeuza DLDB kuwa sehemu za kutolea tiba kwa wagonjwa kulaza wagonjwa, kuchoma sindano n.k

## 1.4: VICHOCHEO VYA MATATIZO YA DLDB

- Upungufu katika vifungu vya sheria kwa kutoshirikisha ngazi za wilaya na kata katika udhibiti na usimamizi.

- Upungufu katika udogo wa adhabu kwa wakosaji

- Ukosefu/kutoruhusiwa kwa dawa za msingi ili kukidhi mahitaji ya jamii

- Kukosekana kwa wauzaji wa jumla wa dawa katika maeneo jirani na DLDB

- ❖ Ufahamu mdogo kwa wananchi kuhusu tofauti ya OTC na PoM ikichangiwa na ufahamu mdogo kuhusu madhara ya kutumia ya nusu kozi ya dawa kwa wagonjwa.

- ❖ Kuendesha DLDB kibiashara zaidi bila kuzingatia kutoa huduma kwa wagonjwa n.k

# 1.5: Mchango wa DLDB katika sekta ya Afya

Pamoja na matatizo mengi yaliyotajwa hapo awali:-

- ✓ DLDB yanaendelea kuwa maduka pekee yaliyoenea sehemu zote nchini na kuwa tegemeo kwa wananchi kwa ajili ya ushauri na dawa.
- ✓ Kutoa ajira binafsi
- ✓ Kuchangia katika kutoa elimu ya afya kwa umma

## 1.6 Changamoto

"Kutokana na kuwepo kwa mtandao (network) mkubwa wa DLDB ni dhahiri kuwa mpango wa kuboresha utoaji huduma na upatikanaji wa dawa katika maduka ya dawa baridi utakuwa ni ukombozi kwa usalama na afya za watanzania" – Hima tushiriki sote katika kuboresha Maduka ya Dawa Baridi.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA